
# Mitizamo ya Viongozi wa Biashara juu ya Mazingira ya Uwekezaji Tanzania 2011




BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy

2012

## YALIYOMO


1. **Muhutasari**...... uk 3
2. **Thathmini ya mazingira wezeshi**......uk 5
3. **Mantiki ya utafiti huu**...... uk 6
4. **Mbinu za utafiti** ...... uk 7
5. **Maelezo ya jumla** ....... uk 8
6. **Mapitio kwa eneo** ..... uk 13
7. **Gharama za urasimu** ..... uk 14
8. **Matokeo ya utafiti ya ziada** ... uk 13


## UTANGULIZI

Hii ni ripoti ya nne ya kila mwaka ya viongozi wa biashara nchini Tanzania. Inatoa muhutasari wa maoni yao juu ya mazingira wezeshaji na nafasi ya serikali katika kuhakikisha biashara zinafanywa kwa urahisi. Ripoti hii imeandaliwa ili kumulika vipaumbele vya kuchukuliwa hatua kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia biashara Tanzania. Utafiti huu iligharimiwa na BEST-AC asasi ambayo majukumu yake ni kuzizaidia asasi za sekta binafsi (PSOs) kujihusisha katika mazungumzo kati ya sekta binafsi naya umma kwa lengo la kushawishi mabadiliko kwenye sera za umma kwalengo la kuboresha mazingira ya biashara Tanzania.

Benki ya Dunia inaeleza kuwa maboresho kwenye mazingira wezeshajii huongeza kiasi cha uwekezaji wa sekta binafsi,ongezeko la utajirisho na ajira na kwa maana hiyo, itasaidia kupunguza umaskini.Njia nzuri ya serikali kuelewa namna ya kuboresha mazingira wezeshaji kwa bishara ni kuwa na mazungumzo na mashauriano, na hasa kuelewa na kushughulikia mahitaji na vipaumbele vya sekta binafsi.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa mitazamo ya viongozi wa biashara haijabadilika sana kati ya mwaka 2009 na 2011, hali inayoakisi pia tathmini ya Benki ya Dunia juu ya utafiti wake wa Ufanyaji Biashara (Doing Business).

Kazi ya kukusanya taarifa za utafiti huu zilifanywa na Synovate kati ya Juni na Julai, 2011. Majibu yake yalifanyiwa uchambuzi na ripoti iliandikwa na David Irwin.

**© BEST-AC 2011**

Katuni ukurasa wa kwanza imechorwa na Abdul Kingo

# Mitizamo ya Viongozi wa Biashara juu ya Mazingira ya Uwekezaji Tanzania – 2011

## 1. MUHUTASARI

Viongozi wa biashara waliulizwa juu ya mambo yafuatayo:


- Mambo muhimu yatakayoleta mazingira mazuri kwenye biashara zao;
- Vitu vinavyofanya biashara yao iwe ngumu;
- Vikwazo visivyokuwa vya kodi ambavyo ni muhimu kwenye biashara zao;
- Vikwazo visivyokuwa vya kodi vinavyoleta matatizo kwenye biashara zao;
- Mitizamo yao kama serikali inashungulikia kila kipengele na kama ndio, inashukighulikia vipi.
- Mawazo yao kama kila kipengele kinaweza kukwamisha uwekezaji kwa siku za baadaye; na
- Tathmini ya gharama inayohitajika kukidhi mahitaji yanayotakiwa kisheria na kiurasimu.

Utafiti huo unaonyesha kuwa mambo yanayoleta ugumu katika kuendesha biashara na kuzifanya zikue kama inavyotakiwa ni pamoja na:-

- Umeme
- Barabara
- Rushwa
- Maji


Umeme umekuwa ni tatizo la mara kwa mara na barabara ikiwa nafasi ya pili. Rushwa, ambayo ilionekana kupungua mwaka 2010, imerudi tena na kuwa ni tatizo kubwa. Maji ambayo hayakutajwa kuwa ni tatizo hadi mwaka 2010, sasa linaonekana kuwa katika hali mbaya. Upatikanaji wa fedha umeshuka kidogo, ingawa watunga sera wasibweteke kwa sababu bado ni tatizo.

**Kielelezo 1: Mambo yanayofanya biashara iwe ngumu kwa ukubwa wake**




Utafiti huu unaangalia mitizamo iwapo serikali inafanya jitihada kushughulikia kila moja ya vipengele hivi. Ugumu unaosababishwa na kila kipengele na mitizamo wa kiasi cha jitihada zinazofanywa na serikali kushughulikia tatizo huunganishwa na kutoa "faharasi ya mazingira yenye kipaumbele." Tambua kuwa kwenye kielelezo hapa chini kadiri namba inavyokuwa ndogo ndivyo kipaumbele cha kushughulikia kipengele husika kinavyokuwa cha juu.

**Kielelezo 2: Faharasi ya mazingira yenye kipaumbele**




Masuala ambayo serikali inatakiwa kuyapa kipaumbele kulingana na umuhimu wake yameonyeshwa kwenye safu ya kulia ya kielelezo namba 3 ambacho pia kinaonyesha jinsi vipaumbele vilivyobadilika tangu mwaka 2008. Nishati na rushwa vinaendelea kuongoza kwenye orodha hiyo. Maji yanazidi kuwa na kipaumbele. Barabara zikibakia kuwa muhimu.

**Kielelezo 3: Kubadilika kwa mambo ya kipaumbele**





Kutokuwepo kwa kipengele chochote kwenye orodha hii haimaanishi kuwa serikali ikipuuzie, bali inamaanisha kuwa serikali imekuwa ikifanya jitihada kupunguza athari mabaya kwa biashara. Hivyo jitihada zinatakiwa ziendelee vinginevyo kinaweza kuwa kipaumbele muhimu kwa siku za baadaye. Ifahamike kwamba hizi ni nafasi siyo alama, kwa hiyo tofauti kati ya kipengele kimoja na kingine inaweza kuwa ndogo sana.

## 2. THATHMINI YA MAZINGIRA WEZESHI

Benki ya Dunia hutafiti viashiria mbalimbali na kisha huchapisha ripoti yake ya kila mwaka inayojulikana kama "Doing Business"[1].

Ripoti hiyo ya Doing Business hugusia viashiria vichache tu. Nchi nyingi zimekuwa zikichukua hatua kutokana na matokeo ya ripoti hiyo kwa lengo la kupunguza urasimu na kuleta mabadiliko. Hata hivyo, inawezekanai kujikita kwenye viashiria viwili, vitatu tu na ukaleta na mabadiliko makubwa kwenye uwepesi wa kufanya biashara (yaani kwenye nasasi zao kwenye orodha) kwa hiyo mitizamo ya sekta binafsi inaweza kuwa kwamba hakuna mabadiliko makubwa yaliyotokea.

**Kielelezo 4: Nafasi za nchi kwenye ripoti za Doing Business**




Chanzo: Imechukuliwa kutoka kwenye ripoti mbaliza Benkiya Dunia za: Doing Business 2009 (2008), Doing Business 2010: reforming through difficult times (2009), Doing Business 2011: Making a difference for entrepreneurs (2010), Doing Business 2012: Doing business in a transparent world (2011).

Ripoti ya Doing Business 2012, inaiweka Tanzania kwenye nafasi ya 127, nafasi ambayo haitofautiani sana na mwaka jana. Kusema kweli, nafasi yake katika maeneo muhimu ya kufanya biashara nayo imebakia pale pale.

Pengine inaleta maana zaidi kuzilinganisha jitihada za Tanzania na nchi nyingine kwenye ukanda huu. Kulingana na ripoti yaDoing Business ya mwaka 2010, Rwanda ilishika nafasi ya kwanza kwa mwaka 2009 ambapo ilipanda kwa nafasi 76; na kwa mwaka 2010 ilishika nafasi ya pili kwa kuleta mabadiliko, ambapo ilipanda kwa nafasi 9. Tanzania imebakia karibu pale pale kwa nafasi za jumla (kielelezo 4) na kwenye nafasi ya kwake (Jedwali 1).

Pamoja na kwamba ripoti za Benki ya Dunia zina thamani kwa watunga sera kutokana na kumulika maeneo yanayohitaji kufanyiwa mabadiliko na kuibua mijadala, bado hazitoi picha kamili. Zaidi ya hayo, kuwahimiza watu wengi zaidi kuazisha biashara au kujiingiza kwenye uchumi rasmi kutategemea zaidi mitizamo mipana juu ya urahisi wa kufanya biashara kuliko kutegemea ripoti finyu inayotolewa kwenye Doing Business.

[1] World Bank, Doing Business: see www.doingbusiness.org

**Jedwali 1: Nafasi ya Tanzania kwenye Doing Business**

| | 2008 (DB 2009) | 2009 (DB 2010) | 2010 (DB 2011) | 2011 (DB 2012) |
|---|---|---|---|---|
| Urahisi wa kufanya biashara | 126 | 131 | 128 | 127 |
| Kuanzisha biashara | 109 | 120 | 122 | 123 |
| Kushughulikia leseni | 172 | 178 | 179 | 176 |
| Kusajili mali | 142 | 145 | 151 | 158 |
| Kulipa kodi | 109 | 119 | 120 | 129 |
| Mikataba ya kisheria | 33 | 31 | 32 | 36 |
| Biashara nje ya mipaka | 103 | 108 | 109 | 92 |


Chanzo: Benki ya Dunia(2008), Doing Business 2009; World Bank (2009) Doing Business 2010: reforming through difficult times (Tanabahi: Nafasi ya mwaka 2009 ilirekebishwa kwenye ripoti ya 2010); Benki ya Dunia (2010), Doing Business 2011: making a difference for entrepreneurs (Tanabahi: Nafasi ya mwaka 2010 kwenye kipengele cha 'urahisi wa kufanya biashsra' ilirekebishwa kwenye ripoti ya mwaka 2011 ili kuakisi mabadiliko madogo kwenye vipengele na masahihisho ya takwimu, ambapo ilishika nafasi ya 125); Benki yaDunia (2011), Doing Business 2012: kufanya biashara kwa uwazi zaidi (Tanabahi: Nafasi ya mwaka 2011 ilirekebishwa kwenye Doing Business, ripotiya 2012, na matokeo ni kwamba Tanzania

## 3. MANTIKI YA UTAFITI HUU

Kutokana na tafiti zinazofanywa na mashirika kama Benki ya Dunia na Jukwaa la Kiuchumi Duniani ( World Economic Forum), inaweza kuonekana kama hakuna tena haja ya kufanya utafiti kutathmini matatizo yaliyopo kwenye biashara. Hata hivyo utafiti huu uko tofauti:

- Mitizamo na hali halisi vinaweza kuwa tofauti, lakini watu hufanya mambo yao jinsi wanavyoona hata kama wanachkioona hakiko sahihi kwa ujumla wake. Si tu kwamba uelewa wa mitizamo utawashawishi watunga sera kwamba kuna mambo zaidi wanatakiwa kuyafanyia kazi, bali pia pale kwenye tofauti kubwa kati ya mitizamo na hali halisi, kutaipa serikali vidokezo jinsi ya kuwasilisha ujumbe wa hali halisi.
- Utafiti huu unavitenganisha vipengele ambavyo ni muhimu kwa sekta mahususi. Kuna vipengele vingi ambavyo kwa pamoja vinaunda mazingira wezeshaji kwenye biashara, ingawa si vipengele vyote ni muhimu kwa kila biashara, na siyo vyote vinasababisha ugumu katika kufanya biashara. Kipengele ambacho ni muhimu katika biashara siyo lazima kichangie kuleta ugumu katika kufanya biashara, ingawa tunaweza kutarajia kuona mambo yanayoendana.

Katuni imechorwa na Cloud Chatanda



- Utafiti huu unauliza siyo tu juu ya vipengele vinavyoleta matatizo, bali pia tofauti na tafiti nyingine, inawauliza viongozi wa bishara kuainisha vipengele ambako serikali inaonekana kufanya kazi nzuri.
- Utafiti huu unauliza pia juu ya vipengele ambavyo kwa siku za baadaye vinaweza kuzuia uwekewzaji. Kuna hatari kuwa serikali inaweza ikachukulia kuwa biashara inaweza ikaendelea hata kama kutakuwa hakuna mazingira mazuri, lakini matokeo ya utafit huu yanaonyesha kuwa hali haiko hivyo.
- Utafiti huu umejaribu kuainisha gharama zinazowakabili ili kukidhi mahitaji ya kisheria yanayowekwa kwenye biashara.

Pamoja na utafiti huu wa nne unaashiria kuwa maeneo ya vipaumbele yamebadilika kidogo, kwa sehemu kubwa unathibitisha vipaumbele vilivyoainishwa mwaka jana. Kwa maana hiyo haya yanapaswa kuwa maeneo ya kipaumbele kwa serikali kuchukua hatua kama inataka kuleta mabadiliko siyo tu kwenye mazingira wezeshi, bali jinsi inavyochukuliwa na watu wanaofanya biashara.

Tanzania kwa sasa imekuwa ikifanya jitihada kubwa ili kuboresha nafasi yake kwenye ripoti ya Doing Business na imekuwa ikitafuta mawazo na taarifa bora zaidi kutoka sekta binafsi. Serikali na sekta binafsi zinaonekana kuja pamoja na kufanya mazungumzo na kushirikiana katika kuandaa sera na kukubaliana katika baadhi ya sera,ambazo, inatarajiwa, zitasaidia kuboresha mazingira ya kufanya biashara na hatimae kuwa na uwekezaji, ajira na mapato zaidi ya kodi. Utamaduni uliojengeka kwenye wizara mbalimbali umeanza kubadilika, ingawa hakuna nafasi ya kubweteka. Sekta binafsi inahitaji kuupokea vizuri uwazi huu wa serikali.

# 4. MBINU ZA UTAFITI

Kazi ya kukusanya taarifa kwa ajili ya utafiti ilifanywa na Synovate, taasisi ya kimataifa inayojihusisha na utafiti wa masoko, kati ya Juni na Julai 2011 na.

Utafiti huu uliendeshwa kwa kutumia dodoso la kieletroniki lililoandaliwa na David Irwin. Synovate ikaweka kwenye Spreadsheet matokeo ya kila aliyejibu maswali hayo. Matokeo hayo yalifanyiwa uchambuzi na David Irwin.

Waliohusishwa kwenye utafiti huo ilikuwa ni biashara 157 zikihusisha sekta, maeneo na ukubwa mbalimbali.

**Jedwali 2: Sampuli ya idadi ya watu**


| Sekta | | Eneo | | Ukubwa (wafanyakazi) | |
|---|---|---|---|---|---|
| Huduma | 27 | Dar es Salaam | 127 | 0-9 | 58 |
| Kilimo & Usindikaji | 29 | Arusha | 30 | 10-24 | 51 |
| Viwanda | 25 | | | 25-49 | 17 |
| Hoteli & utalii | 28 | **BMO** | | 50-99 | 17 |
| Fedha | 25 | Mwanachama | 77 | 100-250 | 8 |
| Mawasiiano | 23 | Asiye mwanachama | 80 | >250 | 5 |
| | | | | Hakusema | 1 |

# 5. MAELEZO YA JUMLA

Katika swali la kwanza, wahojiwa walitakiwa kuonyesha vipi kati ya vipengele kadhaa vilikuwa muhimu katika kufanikisha biashara yao, na baada ya hapo walitakiwa kuonyesha kama kipengele husika kilikuwa kinaleta ugumu mkubwa katika kufanya biashara, ugumu kiasi, palikuwa na uwezekanao wa maboresho au hapakuwa na tatizo kabisa. Sababu ya kugawanya matokeo ni kwamba inawezekana kabisa kipengele kikawa ni muhimu - kwa mfano; mzalishaji anaweza kuwa anahitaji chanzo cha umeme cha uhakika au biashara ya huduma inaweza ikawa inahitaji mawasiliano ya simu ya uhakika - lakini kipengele hicho kisiwe tatizo – umeme au mawasiliano ya simu yanaweza kuwa yanapatikana kwa uhakika. Vile vile baadhi ya vipengele vinaweza visiwe vya muhimu – tunaweza tukatarajia, kwa mfano, kwamba rushwa inaweza ichukue alama ya chini kwa umuhimu, isipokuwa kama biashara hiyo inategemea rushwa ili ifanikiwe - lakini inaweza kuingilia ufanisi wa usimamizi na mafanikio ya biashara.


Vipengele vingi vinaonekana kwa ni muhimu. Kusema kweli, ukiondoa rushwa,vipengele vyote vinaonekana kuwa muhimu kwa asilimia 75 ya wahojiwa. Vipengele vinne – yaani umeme, barabara, mawasiliano na ulinzi – vilionekana kama muhimu kwa asilimia 95 ya waliohojiwa.

**Kielelezo 5: Umuhimu wa vipengele (wahojiwa wote)**




Viongozi kwenye biashara waliombwa kuvipanga vipengele kulingana na jinsi vinavyosaabisha 'ugumu sana wa kufanya biashara', 'ugumu kiasi wa kufanya biashara', 'vinaweza kuboreshwa' au 'havina matatizo'. Majibu yamealamishwa kwa kupewa maksi kwa kila jibu (kuanzia 1: havina tatizo hadi 4: husababisha ugumu mkubwa kuendesha biashara) na baada ya hapo yakatafutiwa wastani. Hii inaonyesha kuwa masuala makuu ni umeme, barabara, rushwa na maji.

**Kielelezo 6: Vipengere vinavyofanya uendeshaji biashara kuwa mgumu**




Katuni imechorwa na Paul Ndunguru





Wahojiwa waliulizwa iwapo walikuwa ni wananachama wa chama cha kibiashara (BMO). Katika miaka iliyopita pamekuwa na tofauti ndogo katika mitizamo baina ya wafanyabiashara wenye uanachama na wale wasio wanachama. Hata hivyo kwa mwaka 2011, isipokuwa kwa umeme, inaoneka kuwa vipengele vingi vinaonekana kuwa na ugumu kwa wanachama. Lakini bado haijaeleweka vizuri kwa nini hali iwe hivyo – je, biashara nyingi zinajiunga na vyama kwa kuwa zina dukuduku sana juu ya masuala haya na zinataka malalamiko yao yasikike, au wanachama wa BMOs wao wako makini zaidi kwenye masuala haya kwa sababu yanajadiliwa na BMO? Hii inaweza kuwa mada nzuri kwa utafiti zaidi.

**Kielelezo 7: Mitizamo ya vipengele vyenye ugumu kwa wanachama wa BMO**





Swali moja liliuliza juu ya madhara ya vikwazo visivyo vya kodi. Inaonekana umuhimu wa vikwazo visivyo vya kodi umeshuka tangu mwaka 2010.

**Kielelezo 8: Umuhimuwa vikwazo visivyo vya kodi (Kwa wahojiwa wote)**



Ingawa vikwazo vyote vitanob vinachukuliwa na wafanyabiashara wachache kuwa vinachangia kufanya biashara kuwa ngumu, kwa wahojiwa wengi havikuwa tatizo hata kidogo.

**Kielezo 9: Vikwazovisivyo vya kodi (NTBs) ambavyo vinaleta ugumu kwenye biashara**





Majibu hayo yanapoalamishwa na kuwekwa pamoja, inaonekana kuwa wahojiwa wanafikiri kuwa vingengele vyote hivyo vinaweza kuboreshwa, ingawa vituo vya mizani barabarani si tatizo sana. Ukiondoa taratibu za uhamiaji, vikwazo vyote vinaonekana kutokuwa na ugumu ikilinganishwa na mwaka 2010.

Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kuwa wakati vikwazo visivyo vya kodi vinaweza kuwa ni tatizo kwa idadi ndogo ya biashara, vinaweza kuwa ni tatizo kubwa kwa biashara hizo na kuleta athari kubwa – kwa mfano vikwazo vinavyozuia ugawaji kwa njia ya barabara au vinaongeza urasimu katika kusafirisha bidhaa nje, vinaweza kusababisha ucheleweshaji kwa wasanidi au wasindikaji lakini wanaweza wao wasiligundue hilo kwenye tathmini yao wenyewe ya mazingira. Vinaweza pia kuwa na athari ambayo haina uwiano kwenye biashara za kimataifa.

Kuna tofauti za kuvutia kati ya wahojiwa wa Arusha na wale wa Dar es Salaam. Kwa ujumla biashara nyingi Dar es Salaam zinaona kuwa mazingira ya biashara yana ugumu ukilinganisha na zile za Arusha. Lakini kwa vikwazo visivyo vya kodi, biashara za Arusha ndizo zenye kupata ugumu zaidi. Taratibu za uhamiaji zinaonekana kufanya uendeshaji biashara kwa kiasi fulani kuwa mgumu. Na wahojiwa wa Arusha wako wazi zaidi kuwa taratibu za forodha na viuizi vya polisi barabarani vinaweza kuboreshwa.

**Kielelezo 10: NTBs ambavyo vinafaya kuwe na ugumu kwenye biashara**





Wahojiwa waliulizwa juu ya mitizamo yao kuhusu jitihada za serikali kushughulikia masuala haya ili kuweka maingira mazuri ya biashara. Majibu yalianzia kutoka yale yanayosema kuwa serikali inafanya jitihada kwa kushughulikia masuala haya (iliyopewa alama 1), kwenda kwenye 'inaonyesha jitihada', 'haifanyi jitihada yoyote' hadi ile inliyosema kuwa 'serikali inafanya mambo yawe magumu zaidi' (iliyopewa alama 4). Majibu yakiwekwa pamoja kwenye alama moja yanaonyesha kuwa kuna vipengele vichache ambapo wahojiwa wanaona kuwa serikali

imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kuleta mabadiliko, japo, kama ilivyokuwa mwaka 2010 mawasiliano ya simu yalionekana kuwa na matokeo mazuri na kwa vipengele vingi ilionekana kuwa serikali ilikuwa ikifanya angalau jitihada kidogo.


Pengine inafaa kuzingatia kuwa hali siyo hivyo kwa kipengele cha umeme, ambapo kuna imani dhahiri kuwa serikali haifanyi jitihada yoyote. Wakati hapajawa na mabadiliko malubwa kwenye mitizamo inayohusiana na rushwa,kuna mtizamo pia kuwa serikali haijafanya juhudi za maana kwenye eneo hilo.

**Kielelezo 11: Utendaji wa serikali katika kushughulikia vipengele mbalimbali**





Tunaweza kutarajia kuwa biashara ambazo ni wanachama wa BMO zingekuwa wakosoaji wakali zaidi wa serikali na jitihada zake za kuleta mabadiliko kwa kuwa moja ya sababu za biashara kujiunga na vyama ni kupigia debe mabadiliko ya sera za umma. Ni jambo la kuvutia kuona kuwa kuna tofauti ndogo ya mitizamo kwa vingele vingi. Vipengele vinavyojitokeza zaidi ni umeme – ambapo wanachama wanalikosoa zaidi jambo hilo – na rushwa – ambapo wanachama wanaikosoa zaidi serikali.

**Kielelezo 12: Mitizamo juu ya jitihada za serikali kwa wanachama wa BMO**



Wahojiwa waliulizwa ni vipengele vipi vina uwezekano mkubwa wa kushawishi maamuzi ya uwekezaji na kwa vipi (alama 1: inahimiza uwekezaji zaidi; 2: haihimizi wala kukwaza; 3: inakwaza uwekezaji zaidi). Katika miaka michache iliyopita, rushwa imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa uwekezaji, lakini kwa sasa nafasi yake imechukuliwa na umeme. Nishati na rushwa zote zilipata zaidi ya alama 2 kwa hiyo ni vipengele ambavyo vinaweza kukwaza uwekezaji kwenye sekta nzima ya binafsi,


**Kielelezo 13: Vipengele vinavyoathiri maamuzi ya uwekezaji Usalama**





Tumeandaa 'faharasi ya mazingira yenye kipaumbele'. kwa kuangalia ugumu kwenye biashara ukichanganya na mitizamo ya jinsi serikali inavyoshughulikia suala husika.

Chati hapo chini inaonyesha majumuisho ya maoni kwa vipengele vyote vinne. Zingatia kwamba kwenye jedwali hili kipimo kimegeuzwana na kupangwa upya ili kipengele ambacho kinasababisha ugumu zaidi kwenye biashara na ambapo serikali inazidi kuboronga ,kitaonyeshwa kama sifuri na kipengele ambacho kinaleta ugumu kidogo kwenye biashara na serikali inafanya jitihada zaidi kukiboresha kitaonyeshwa kwenye nafasi ya 100. Kwa hali hiyo, kipengele kinachoonekana kuwa na matatizo madogo zaidi ni mawasiliano ya simu, ikifuatiwa na ulinzi na sheria ya kazi; na kipengele ambacho ni tatizo kubwa zaidi ni umeme ukifuatiwa na rushwa, maji na barabara.

Katuni imechorwa na Cloud Chatanda



**Kielelezo 14 : Orodha ya vipaumbele vya mazingira wezeshi**




Ni vigumu kujumuisha maoni yote kwenye tarakimu moja,lakini tunatambua kwamba kuwa na tarakimu moja kunakusaidia kutambua mara moja iwapo sekta binafsi inaona kuwa mazingira wezeshi kwa biashara yameboreshwa au yamekuwa mabaya zaidi.

Kwa hiyo tukokotoa tarakimu moja – na kuona kuwa kumekuwwpo uzorotaji mdogo sana ikilinganishwa na mwaka 2010. Hata hivyo tarakimu zinakaribiana sana kiasi cha kuamaanisha mitizamo kwamba kwa ujumla pamekuwa na mabadilik kidogo sana.

**Jedwali 3: Orodha ya mitizamo ya mazingira wezeshi**

| | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 |
|---|---|---|---|---|
| **Tanzania** | 57 | 65 | 67 | 63 |
| **Burundi** | | 71 | | |
| **Kenya** | 52 | 56 | | |
| **Rwanda** | | 76 | | |
| **Uganda** | 63 | 59 | | |


Kwa wasomaji ambao wanataka taarifa kwa undani zaidi, BESTAC inaweza kutoa takwimu za kipengele kimojakimoja. Inaweza pia kutoa takwimu kulingana na ukubwa wa asasi.

# 6. MAPITIO KWA ENEO

Tuliwaomba wahojiwa kuelezea maeneo waliko ili tuweze kulinganisha majibu kwa misingi ya eneo la kijiografia, ingawa tuna majibu ya maana kutoka maeneo mawili tu. Kwa ujumla biashara za Dar es Salaam zinaona ugumu zaidi wa kufanya biashara, ingawa matokeo ya utafiti wa 2010 yalikuwa kinyume na hayo.

Hata hivyo, umeme ni tatizo kubwa zaidi Arusha,huku ,kila mhojiwa akisema inafanya uendeshaji biashara kuwa mgumu sana. Maji na upatikanaji wa fedha unachulukiwa kuwa mbaya zaidi Arusha.

**Kielelezo 15: Vipengele kwa maeneo**




## 7. GHARAMA ZA URASIMU

Shirika la OECD (2001, Mitizamo ya wafanyabishara juu ya urasimu: vikwazo vya kiutawala na kikanuni kwenye biashara ndogondogo na za kati) linaeleza kuwa gharama za kiutawala kwa kila mfanyakazi kwa biashara ndogo ni mara tano zaidi ya zile zinazozikabili biashara kubwa. Wanasema kuwa kwa wastani miongoni mwa nchi za OECD biashara ndogo na za kati hutumia $27,000 kukidhi sheria kiasi ambacho ni sawa na $4,100 kwa kila mfanyakazi au asilimia nne ya biashara yote kwa mwaka. Wamechambua zaidi tarakimu hizo na kudokeza kuwa biashara zinazoajiri wafanyakazi kati ya 1-19 hutumia $4,600 kwa kila mfanyakazi kwa mwaka na biashara zinazoajiri watu 20-49 hutumia $1,500 kwa kila mfanyakazi na biashara zinazoajiri watu 50-500 hutumia $900 kwa kila mfanyakazi.





Katuni imechorwa na Adam Lutta

Wahojiwa kwenye utafiti waliulizwa kuhusu gharama za ukidhi wa taratibu –ikigawanywa kwenye makundi matatu: gharama za moja kwa moja za kutafuta leseni pamoja na gharama za leseni zenyewe, muda unaotumika kwa mfanyakazi kushughulikia ukidhi wa taratibu na gharama za muda wa mfanyakazi za kukabiliana na wasimamizi wa taratibu. Hususan wahojiwa walitakiwa kueleza wanaona wao wamo kwenye kundi lipi la gharama


Kwa mwaka 2009, asilimia 20 ya wahojiwa walisema kuwa kulikuwa na gharama kidogo au hakuna gharama katika kila kundi na mtizamo huo ulirudiwa kwa mwaka 2011.

**Kielelezo 16: Gharama ya urasimu na sheria**





Kama ilivyokuwa kwa miaka iliyotangulia wengi wa wahojiwa waliona kuwa kulihitajika matumizi ya chini ya asilimia tatu kwa kila kipengele. Hali hii inaonekana kuwa ni ndogo ingawa unapojumulisha makundi yote matatu, ghafla inaweza kuwa kubwa. Chati hapo chini inaonyesha wastani wa matumizi ya kisekta kwa kila moja ya makundi haya matatu juu ya gharama za ukidhi wa taratibu.

**Kielelezo 17: Gharama ya urasimu na kisheria**




Siyo tu kwamba wanafanya biashara Dar wanaona vipengele vya kurahisisha biashara vinachangia kuweka mazingira magumu ya biashara kuliko Arusha, bali pia wanaona kuwa masuala ya taratibu yanagharimu zaidi.

**Kielelezo 18: Ulinganifu wa kijiografia wa gharama za kisheria**




## 8. MATOKEO YA UTAFITI YA ZIADA KUTOKA SEKTA NYINGINE

Kwenye ripoti nzuri iliyoandaliwa kwa ajili ya Shirikisho la Wahudumu wa Utalii Tanzania[2], waandishi wanadokeza kwamba:

- Mtanzania anayejihusisha na kazi ya kusafirisha watalii anatumia wastani wa saa 745 kwa mwaka (zaidi ya miezi minne) kwenye kufuatilia taratibu za ukidhi na kumgharimu Sh. milioni 2.9.
- Hoteli ya Kitanzania inatumia saa1,042 kwa mwaka (karibu, miezi sita) kwenye taratibu za ukidhi kwa gharama ya Sh. milioni 3.4
- Gharama za kitaratibu za kufanya biashara kwa sekta ya utalii Tanzania inazidi Sh. bilioni.1.1 kwa mwaka.

Waandishi wa ripoti hiyo wanaeleza kuwa gharama hizi kubwa zinaiumiza sekta na mwisho wa siku zinaiumiza serikali.

*Mwafaka wa jumla miongoni mwa Wanafanya biashara ya utalii nchini Tanzania kuhusu vikwazo vya ukidhi wa taratibu ni kwamba idadi na mlolngo wa taratibu una ugumu unaoiumiza sekta hiyo kwa kupunguza faida na kuwakatisha tamaa watu wanaotaka kuingia rasmi, ambapo mwisho wa siku hali hiyo inaiumiza serikali, kwa kushindwa kupata mapato kutoka kwenye sekta hiyo. …taratibu za kupindukia, zimekuwa sababu ya kufilisika kwa biashara nyingi ndogondogo. Zaidi ya hayo,ugumu wa kupata nyaraka za taratibu zilizofanyiwa marekebisho na kutokuwepo kwa usaidizi wa kutosha kufafanua masuala mapya ya leseni, usajili na kodi umezifanya baadhi ya biashara za wenyeji kuendeshwa kinyemela kuliko kujitokeza na kuingia kwenye sekta rasmi ya utalii*




Katuni imechorwa na Fadhil Mohamed

*Kuna haja basi ya kutengeneza uhusiano wa kirafiki wenye maelewano baina ya sekta binafsi na serikali. Serikali ina jukumu la kusimamia biashara, ikihakikisha usalama na hali bora kwa wafanyakazi na watalii na kupata mapato. Hata hivyo lazima pawepo na kuhakakishwa mazingira wezeshajii kwa biashara ya utalii –ambapo gharama ya kufanya biashara imepungua, mzigo wa kiutawala wa kukidhi taratibu umepungua,na watalii wanapata picha nzuri –ili biashara zipate faida,ambayo nayo itaiwezesha serikali kukusanya mapato ya kutosha.*

[2] Raheem, Z & Mkindi, A (2010), "Competitiveness impacts of business environment reform: regulatory constraints to the competitiveness of the tourism sector in Tanzania: platform for advocacy", DAI for TCT

Wanaendelea kueleza kuhusu mzigo unaotwishwa biashara kutokana na urasimu ambao kwa sehemu kubwa si wa lazima, huku wakisisitiza kuwa biashara zinatambuahaja ya serikali kukusanya mapato. Waandishi wanadokeza kwamba biashara nyingi zingefurahi zaidi kulipa kodi na tozo mbalimbali kama mzigo wa kitaratibu ungepunguzwa kwa kiasi kikubwa na kama matumizi ya serikali yangekuwa ya uwazi zaidi.

> *Mzigo mkubwa wa kitaratibu unatwishwa biashara [zote] kujaza nyaraka zote za leseni na kodi kila mwezi, robo mwaka na mwaka. Ukiachia mbali gharama halisi ambazo biashara hulipa, gharama hizi za kiutawala zinageuka kuwa gharama halisi kutokana na muda ambao inabidi utengwe [kwa wafanyakazi] kushughulikia michakato hii — kuzielewa taratibu, kupakua fomu kutoka kwenye mtandao, kuijaza,kuitolea nakala, kupata nakala za wakala wengine wa serikali, kujaza fomu, kupiga photocopy, kupata nyaraka za ziada za kuzithibitisha, kudufurisha nyaraka za idara mbalimbali za serikali, kuziwasilisha nyaraka kwenye ofisi mbalimbali za serikali za mitaa na serikali kuu, kuhakikisha kama zimefika na kuendelea kuzifuatilia kwa wakuu husika wa serikali. Kuwepo kwa mfumo mmoja mwanana zaidi bado kungeiwezesha serikali kupata mapato kutoka kwenye sekta hii huku ikiweka mfumo wenye ufanisi zaidi ambao ungepunguza gharama ya kufanya biashara na kuwapatia wafanyakazi muda kwa kujihusisha na kazi mahususi ya biashara wanayofanya kama vile kutafuta masoko, kutoa mafunzo na kujenga uhusiano na wateja.*
>
> *Biashara zingekuwa tayari kulipa tozo kama tozo hizo zingekuwa kwenye mkondo mmoja wenye uwazi jinsi fedha hizo zinavyotumika. Biashara ya utalii inatambua kuwa wakati wote kuna umuhimu wa kulipa tozo; hata hivyo washiriki wengi kwenye utafiti huu wanaona kuwa kuwepo kwa mchakato wazi na mwepesi zaidi kungeisaidia sketa hii vizuri zaidi.*

Ripoti iliyoandaliwa kwa ajili ya Shirikisho la Viwanda na Biashara nayo inatoa hoja kama hiyo. Inasema kuwa gharama za kiutaratibu (kuandaa nyaraka, kushughulikia forodha, bandari na upokeaji, uchukuzi wa ndani ya nchi bila ushuru) zinazohusiana na kusafirisha nje kontena la futi 20 likiwa na bidhaa zenye thamani ya $20,000 ni $1,262, wakati gharama ya kuingiza kontena kama hilo hugharimu $1,475. Mwandishi pia anataja gharama kwenye tasnia ya maziwa akisema kuwa gharama ya awali ya ukidhi kwa kituo chenye uwezo wa lita 60,000 kwa siku ni kiasi cha TSh. milion 12 na gharama ya ziada ya kila mwaka ya TSh milioni 48.

Urassa na Mchau[3] wanakokotoa kwamba wastani wa gharama isiyokuwa ya moja kwa moja inayohusiana na kuandaa na kuwasilisha maombi, hususan kwa kutumia muda ambao ungeweza kutumika kwa tija zaidi, ni kama Tsh. milioni 48 kwa kila biashara kwa mwaka.

> Kufanya jitihada ya kupunguza gharama za taratibu kungesaidia kuondoa mbano kwa rasilimali ambazo zingeweza kuwekezwa upya kwenye biashara na hivyo kuongeza ajira na michakariko ya kiuchumi na hivyo serikali kupata fedha nyingi zaidi kupitia kodi – kwa hiyo kila mmoja angenufaika.

[3] Urassa, G (2011), "Simplifying compliance of multiple regulatory authorities to enhance the ease of doing business: situational analysis", IMED for CTI.




BEST-AC inazisaidia taasisi za sekta binafsi kujihusisha katika mazungumzo na sekta ya umma ili kuwa na mazingira bora ya kibiashara Tanzania kwa kutoa misaada, mafunzo na ushauri.

**BEST-AC**

**SLP 6983 - Dar es Salaam - Tanzania**

**Simu: (+255) 022 2601168**

**Barua pepe: info@best-ac.org Tovuti: www.best-ac.org**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy